

ARUSHA

FURSA LUKUKI

Endless Opportunities

Toleo la Mtandaoni: 02 Tarehe 06/12/2022



Kazi Iendelea

UTALII, KILIMO, BIASHARA NA UZALISHAJI



OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu



**PONGEZI SANA MHE. RAIS DKT SAMIA SULUHU HASSAN
KWA KUTUNUKIWA SHAHADA YA HESHIMA YA UDAKTARI
WA FALSAFA TOKA CHUO KIKUU CHA
DAR ES SALAAM**



UMUHIMU WA ELIMU YA BIMA NA UHIFADHI WA JAMII BARANI AFRIKA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ameitaka Mifuko ya hifadhi ya Jamii Barani Afrika kuweka mikakati itakayosaidia kuinua uchumi wa watu na kuondoa umaskini.

Ameyasema hayo alipokuwa akifungua Mkutano wa kwanza wa Wakuu wa Mamlaka za BIMA Afrika uliofanyika katika Kituo cha Mikutano Arusha (AICC).

Amezitaka Mamlaka hizo kwa kila Nchi kutoa elimu ya BIMA kwa watu wake kwa kufuata taratibu za Nchi husika ili wananchi waweze kuwa na uelewa

mpana wa maswala ya BIMA

Pia, amezita Mamlaka hizo kuongeza ushirikiano wa Nchi na Nchi ili kuwa na nguvu ya pamoja ya kupambana na mambo mbalimbali yanayojitokeza katika Bara la Afrika hususani mabadiliko ya Tabia Nchi na mradidi mikubwa inayojengwa kwenye nchi za Afrika.

Mhe. Majaliwa amezitaka Mamlaka hizo kuweka mikakati ya kujengeana uwezo wa kitaaluma hususani katika Sekta zinazokingwa na BIMA ilikupunguza changamoto

ya uhaba wa Wataalamu ambao upo kwa sasa katika Nchi nyingi za Afrika.

Amesema jukumu kubwa la mifuko ya BIMA ni kuhakikisha usalama wa Watu, mali zao na mahitaji yao yanalindwa wakati wote majanga yanapotokea kwa kutumia rasilimali zilizopokatika ukanda wa Afrika.

Mkutano huo umejumuishwa Nchi mbalimbali kutoa Bara la Afrika na ukiwa ni Mkutano wa kwanza wa Umoja huo kufanyika.



UKAGUZI WA MRADI WA ELIMU SHULE YA SEKONDARI KETUMBEINE, WILAYANI LONGIDO.

Watumishi wa Umma Mkoa wa Arusha kutoka ngazi zote wametakiwa kujitua kufanya kazi kwa bidii kwenye kusimamia miradi ya maendeleo inayoletwa na Serikali katika Mkoa huo.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha John Mongella wakati wa ziara yake ziara ya kukagua miradi mbalimbali ya Maendeleo katika Wilaya ya Longido.

Mongella amesema, lengo la Serikali ya Awamu ya sita ni kuhakikisha inaondoa kero zinazowakabili Wananchi kupitia miradi hiyo kwani Serikali imekuwa ikileta fedha nyingi za miradi kwa hiyo nguvu ya pamoja inaitajika katika kuhakikisha

miradi hiyo inatekelezeka na kukamilika kwa wakati ili wananchi waweze kupata huduma wanazostahili.

Naye Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha Musa Matoroka amepiongeza Idara ya Elimu Mkoa wa Arusha kwa kusimamia vizuri Miradi ya Elimu na inakamilika kwa wakati.

Hata hivyo, imeitaka idara ya Afya kuongeza kasi ya usimamizi wa miradi yao ambayo bado inasua sua na hivyo kuchelewesha huduma kwa Wananchi.

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa shule ya Sekondari Ketumbeine Esta Kobelo amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muunga

no wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kutatua changamoto ya Wanafunzi kwa kutoa fedha za ujenzi wa Madarasa ili kupunguza msongamano.

Mwl.Kobelo amesema kitendo cha Rais kuongeza Madarasa kimesaidia kuwapingumzia msongamano Wanafunzi ambapo kwa sasa mazingira ya kusoma yameendelea kuboreka na kuwafanya kuwa na amani na uhuru wa kusoma.

Ziara hiyo ya Mkuu wa Mkoa ni mwendelezo wa ziara zake Mawilayani kwa kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayofanyika ndani ya Mkoa ikiwemo Miradi ya Afya, Maji, Umeme na Barabara



OFISI YA MKUU
WA MKOA
ARUSHA

#Utalii Fahari Yetu



Mwonekano wa Mbele wa madarasa matatu mapya ya Shule ya Sekondari Ketumbeine, Wilayani Longido



Viongozi wa Chama na Serikali Mkoa wa Arusha wakiwa katika ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Wilayani Longido.

www.arusha.go.tz



NYUMBA YA WAGENI



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akiteta jambo na Mkuu wa Mkoa wa Arusha John V.K. Mongella



Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K. Mongella akiwa katika mazungumzo na Waziri wa Madini Mhe. Doto Biteko alipofika Mkoani Arusha kwa zara ya kikazi.



Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiteta jambo na Waziri wa Fedha Mhe. Mwigulu Nchemba mara baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Taasisi za Bima Afrika-AICC Arusha.



Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiwa katika mazungumzo na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Anthony Mavunde alipofika kumtembelea ofisini kwake.



Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akisalimiana na Brigedia Jenerali Silvester Damian Ghuliku Mkuu wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu Duluti Arusha-Tanzania mara alipotembelea Chuo hapo



Mkuu wa Mkoa Wa Arusha Mhe. John V.K Mongella akiwa katika picha ya pamoja na Wanadhimu Waelekezi na Maafisa Wanafunzi wa Kozi kundi la 37/22 Chuo cha Ukamanda na Unadhimu Duluti Arusha-Tanzania